LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz
Website www.humanrights.or.tz

# Tamko

## Kukemea Mauaji ya Maafisa misitu na Askari Mgambo

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimepokea kwa masikitiko taarifa za mauaji ya kikatili dhidi ya maafisa misitu pamoja na askari mgambo, mauaji hayo yaliyotokea katika hifadhi ya msitu wa Kijiji cha Chakulu wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma siku ya tarehe 31 Januari, 2023. Tukio la mauaji hayo lilitokea wakati maafisa hao wakiwa kwenye doria ya kuondosha mifugo iliyokuwa imevamia misitu hiyo. LHRC ilipokea taarifa ya tukio hilo mnano tarehe 07 Februari, 2023 kupitia vyombo vya habari.

Tukio hilo ni kinyume cha *Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977* inayoainisha haki ya kuishi.

Hivyo, LHRC inakemea vikali tukio hili la kikatili linalotweza utu wa mtu, Kituo kinatoa wito kwa jamii kuacha vitendo hivyo vya kujichukulia sheria mikononi ambavyo vinapeleka kuumia na kutoa uhai. Ikumbukwe kwamba, maafisa hao ni watu wa muhimu kwa kuwa majukumu yao ni kulinda misitu na mapori tengefu yaliyoainishwa kwa mujibu wa sheria.

Aidha, LHRC inatoa wito kwa vyombo vya dola kuwatafuta, kuwakamata na kuwafikisha watuhumia hao kwenye vyombo vya dola kwa mujibu wa sheria. Pia, Kituo kinatoa wito kwa Serikali kuboresha mahusiano kati ya jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi na maafisa wa uhifadhi ili kuzuia vifo, mapigano pamoja na uharifu wa mali vinavyoweza kuepukika.

Imetolewa leo tarehe 08 Februari 2023 na;

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)

Anna Henga (Wakili)

Mkurugenzi Mtendaji

**Bodi ya Wakurugenzi**

**Mh.Jaji mkuu mstaafu Barnabas A. Samatta - Mwenyekiti, Ms. Anastazia Rugaba – Makamu mwenyekiti, Ms. Anna Aloys Henga (Wakili) Katibu, Ms. Rebeca Z. Gyumi - Mjumbe, Ms. Sophia M. Komba - Mjumbe, Prof. Abdullah H. Mohammed - Mjumbe, Ms. Josephine A. Mwankusye - Mjumbe, Ms. Lutgard Kokulinda Kagaruki - Mjumbe**